
الطريق إلى السعادة
The Path to Happiness




https://www.path-2-happiness.com/sw

# JE, MWANADAMU ANA HAJA YA DINI?

https://www.path-2-happiness.com/sw


https://www.path-2-happiness.com/sw

# Yaliyomo

**JE, MWANADAMU ANA HAJA YA DINI?**

Je, ni lazima kuwa na Dini?

Haja ya dini kwa jamii mbali mbali

Vidhibiti vya dini ya haki

Ni dini ipi tunayohitajia?

# JE, MWANADAMU ANA HAJA YA DINI?


## Je, ni lazima kuwa na Dini?

Mwanadamu kwa hali yoyote hawezi kuishi bila Dini, na kwa sababu mwanadamu ni mtu mwenye tabia ya kuingiliana na watu na hawezi kuishi peke yake huku akijitenga na jamii, nae vile vile katika maumbile yake ni mtu mwenye dini hawezi kuishi maisha ya sawa sawa bila kuwa na dini, swala la mtu kuwa na dini ni suala la kimaumbile na tabia ya asili ya mwanadamu na hakuna dalili kubwa yenye kuthibitisha hilo kuliko ile hali ya mwanadamu kumtegemea Mwenyezi Mungu katika hali ya shida na dharura, Allah Ta'ala amesema, {Na wanapo panda katika marikebu, humwomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafia ut'iifu. Lakini anapo wavua wakafika nchi kavu, mara wanamshirikisha.} [29:65]

### Matokeo Imara

"Imani ni matokeo imara na matukufu zaidi katika tafiti za kisayansi."

**Einstein**
Mwanazuoni wa Fizikia



Kama ambavyo mtu aliyetengeneza mashine ndiye mwenye kufahamu zaidi mahitajio yake vivyo hivyo na muumbaji huwajua zaidi viumbe wake na mahitaji yao, {Asijue aliye umba, naye ndiye Mjua siri, Mwenye khabari? } [67:14]

Na kwa sababu Muumba ni Mrehemu na Ghafuri Mkarimu; amewawekea watu sharia ya Dini ili Nafsi zao zihuishwe na maisha yao yadhibitiwe, Allah Ta'ala amesema, {Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele….} [8:24],



https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw


Na kwa hilo basi hata yule ambaye anakwenda kinyume na maumbile sahihi na anadai kumkana Allah Ta'ala, wao ni ndani ya Nafsi zao wanajua uongo wa kukana kwao, Allah amesema, {Na wakazikataa kwa dhulma na kujivuna, na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo. Basi angalia ulikuwaje mwisho wa mafisadi!} [27:14]

Na huenda hilo likaonekana kwa uwazi zaidi wakati wa zahama na matatizo zaidi, Allah amesema, {Sema: Mwaonaje ikikujieni adhabu ya Mwenyezi Mungu, au ikakufikieni hiyo Saa - mtamwomba asiye kuwa Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi ni wakweli? Bali Yeye ndiye mtakaye mwomba, naye atakuondoleeni mnacho mwombea akipenda. Na mtasahau hao mnao wafanya washirika wake.} [6:41-42]

Kadhalika katika Surat Zumar amesema: {Na taabu inapo mfikia mtu humwomba Mola wake Mlezi naye ameelekea kwake. Kisha akimpa neema kutoka kwake, husahau yale aliyo kuwa akimwitia zamani, na akamfanyia Mwenyezi Mungu washirika ili apoteze watu njia yake. Sema: Starehe na ukafiri wako kwa muda mchache. Kwani hakika wewe utakuwa miongoni mwa watu wa Motoni. } [39:8].

Wanadamu wote wapo katika maumbile ya asili waliyoumbwa nayo na Allah Ta'ala katika kumuabudu yeye kwa mkono wake kheri na shari kufanya ayatakayo na kuhukumu atakavyo, Allah Ta'ala amesema: {Na ikiwa Mwenyezi Mungu akikugusisha madhara, basi hapana wa kukuondolea hayo ila Yeye. Na ikiwa akikugusisha kheri, basi Yeye ndiye Mwenye uweza wa kila kitu.} [6:17]

Na katika Surat Faatwir amesema: {Rehema ambayo Mwenyezi Mungu anawafungulia watu hapana wa kuizuia. Na anayo izuia hapana wa kuipeleka isipo kuwa Yeye. Naye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.} [35:2].



## Mtu wa Dini na Mgonjwa

"Nakumbuka yale masiku ambayo hakukuwepo na mazungumzo ya watu isipokuwa kuhusu ugomvi baina ya elimu na dini. Mgogoro huu uliisha bila kurejewa, kwani elimu ya sasa ya tiba ya nafsi inatoa habari nzuri kuhusu misingi ya dini. Kwanini?!! Kwa sababu matabibu wa nafsi wamegundua kuwa kuwa imani yenye nguvu na kushikamana na dini na swala hutosheleza kushinda wasiwasi, khofu na msongo wa mawazo na kutibu nusu ya maradhi ambayo tunayoyalalamikia. Hadi Dr. A. A. Bell akasema: "Kuwa mtu mwenye kushikamana na dini hasumbuliwi na maradhi ya nafsi."

**Dale Carnegie**

Mwandishi wa Kimarekani.



**Dale Carnegie**
Mwandishi wa Kimarekani

### Kuwa Mbobezi

"Mwanafalsafa Francis Becon alisema kweli aliposema, "Falsafa ndogo humpelekea mtu kwenye kumkana Mungu. Ama kubobea katika falsafa humrejesha mtu kwenye dini."

Mwanadamu ana nguvu za aina mbili: Nguvu ya elimu na nguvu ya matakwa yake, na kwa kadiri ya juhudi yake katika kutekeleza nguvu hizo mbili mwanadamu huyo hufikia malango yake aliyojipangia na vivyo hivyo ndivyo mwanadamu apatavyo furaha.

Ama nguvu ya kwanza (nguvu ya elimu) kwa kadiri ya maarifa yake kwa Allah, kwa majina yake na sifa zake, na yanayopasa kwake katika maamrisho na makatazo, kitabia na kimaadili na vipi ilivyo njia ya ukuruba na kuwa juu ya daraja za mwenye kufuata, na yote yenye kupelekea katika elimu ya ndani kuhusu Nafsi za wanadamu na maradhi yake na jinsi ya kuyashinda hayo, na kwa maadui zake na kila chenye kuzuia baina yake na Mola wake, mbali na mtu kukwea daraja za juu za kutakasa tabia yake iwe ya kiungu kiasi cha kupanda juu kufikia roho za juu na hima za juu, mbali kabisa na mambo ya hovyo kwa lengo la kupata maslahi ya kidunia na matamanio yake, kwa kiasi hicho ndio kimada unapokuwa daraja ya uja wa mtu kwa Allah Ta'ala na nafasi yake, bali na furaha yake duniani sembuse ya akhera.




https://www.path-2-happiness.com/sw

Nguvu hii ya kielimu ndio masurufu na msaada wa nguvu ya matakwa ya mtu, ambayo yatamuongoza katika uongofu pamoja na kuthibiti na kufanya mambo mazuri, Allah Ta'ala amesema: {Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele….} [8:24]

Na haya madhehebu ya wakanayo Mungu na Dini yanatangaza kufilisika kwao kwa kutekeleza kwao raha za kiwiliwili sembuse kushibisha mahitajio ya kiroho, madhehebu haya yameshindwa kabisa kumhakishia mwanadamu furaha ya kweli vyovyote watakavyopeana kauli nzuri na kupamba kauli zao kwa ghururi.

Mwanadamu anamuelekea nani katika matatizo yake na misiba yake! Anategemea nguzo imara, anaelekea kwa Allah Ta'ala; penye nguvu, matarajio, subira na kutegemea kwema na kumwachia mambo yote yeye. Allah amesema; {Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!} [13:28].

Hadi hapo atakapoonja uchungu wa moto kwa dhulma ndipo atakapokuwa na yakini kuwa ulimwengu huu una Mola, na ambaye anamnusuru aliyedhulumiwa hata kama, ni baada ya muda kupita, na ya kuwa kuna siku ya mwisho ambayo kila mmoja atalipwa alichokichuma, na mtu mwema kulipwa mema yake na muovu kulipwa maovu yake na hivyo basi kifua chake kuwa imara kwa tumaini na yakini kwa Allah. Allah Ta'ala amesema: {Je! Aliye yafuata ya kumridhisha Mwenyezi Mungi ni kama yule aliye stahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, na makaazi yake yakawa Jahannamu? Napo ni mahala pabaya pa kurejea.} [3:162].



## Ukweli Ulio wazi Zaidi

"Utafiti wangu kwa ajili ya kupata shahada ya uzamifu (PhD) ilikuwa kuhusu Malezi na kujenga Ummah. Nimegundua kuwa nguzo za Kiislamu za msingi zimeweka misingi mikuu na kanuni madhubuti ili kurudisha jengo la Ummah kijamii, kiuchumi na kiroho

**Dr. Douglas R. Archer**
Meya wa Regina



https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw



## Kushika Dini ni tiba ya Maradhi

"Matabibu wa nafsi wamegundua kuwa imani madhubuti na kushikamana na dini inamtosha kushinda khofu, wasiwasi na msongo wa nafsi na kuponya maradhi haya."


**Dale Carnegie**
Mwandishi wa Kimarekani.

## Tibu mwenyewe nafsi yako.

"Kwa hakika tiba kubwa zaidi ya nafsi ni kumuamini Mwenyezi Mungu."

**William James**
Mwanazuoni wa Elimu nafsi (Saikolojia) wa Marekani.






## Havipo pamoja

"Madhehebu ya Kiyakinifu (unaotanguliza anasa za dunia) siku zote wanathibitisha ambacho wanashirikiana baina ya mwanadamu na mnyama. Wakati ambapo dini inasisitiza kinachotenganisha baina yao."

**Alija 'Ali Izetbegovic**
Rais wa zamani wa Jamhuri ya Bosnia Herzegovina.

Kinyume na yaliyotangulia; yule ambaye amepoteza maarifa yake kwa Allah Ta'ala na kumuamini basi mtu huyo amepoteza nguvu zake zote, na kadhalika atakuwa amepoteza raha, tumaini na furaha, na atakuwa anaishi baina ya hamu na huzuni, hana utulivu ndani ya nafsi yake, hamu yake kubwa ni kutekeleza na kufanikisha matamanio yake hajui malengo ya maisha yake, wala maana ya kuwepo kwake hapa ulimwenguni. Bali mtu huyu anaishi akibabaika hajui afanye nini, akitafuta furaha, akifuata matamanio yake, lakini anarudi nyuma kiasi cha kuwa ni mnyama au aliyepotea zaidi, Allah Ta'ala amesema: {Au wewe unadhani kwamba wengi wao wanasikia au wanaelewa? Hao hawakuwa ila ni kama nyama hoa tu, bali wao wamepotea zaidi njia.}[25:44],

Na ikitokea mtu huyu kapatwa na msiba basi kuangukia kuwa ni muhanga wa angamizo la nafsi na angaiko na babaiko lake la






ndani, {Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu.} [20:124]

Ni tofauti kubwa sana baina ya mtu mwenye kumjua Mola wake, na kujua ukubwa wake na akajua kinachompasa kwake kwa Mola wake na kuijali kwake kumridhisha Mola wake, akifuata sheria zake, akitii maamrisho yake na kuacha makatazo yake, Na akajua kuwa ni mwenye haja ya kudumu kwa Mola wake katika madogo na makubwa, katika mambo dhalili na matukufu, na

## Matabibu wenye kutoa mawaidha



"Kwa hakika matabibu wa nafsi ni watu wenye kutoa mawaidha kwa njia mpya; Kwani wao hawatuhimizi dini kwa sababu ya adhabu ya motoni huko akhera, bali wao hutuusia kushikamana na dini ili tusipate adhabu ile ile ya moto hapa duniani, kama vile moto wa vidonda vya tumbo na msongo wa nafsi na wendawazimu."


**Henry Ford**


Mwanzilisi wa Shirika la Ford la Magari Marekani



https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw





katika kila wakati Allah Ta'ala amesema: {Enyi watu! Nyinyi ndio wenye haja kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujitosha, Msifiwa.}[35:15].

Na mtu mwingine dhana na mawazo yamemtupa katika taabu na kiza na shida, akipapasa kwa kupepesuka kama vile kipofu hapa na pale, moyo wake ukiwa umejaa shaka na wasiwasi, kila akijaribu kukamata au kushika furaha anajikuta yupo katika mazigazi baada ya mazigazi, na hata akipata ladha za dunia na matamanio yake, na hata akipanda cheo na daraja za juu, Je, mtu atakayemkosa Allah atapata nini? Na atakayempata Allah atakuwa amekosa nini?

## Dini ni Maisha

"Dini ni katika vipaji muhimu vya mwanadamu. Tunatosheka kusema kuwa mtu kukosa dini humsukuma kwenye hali ya kukata tamaa kiroho, inamlazimisha kutafuta nguvu ya kidini kwenye sahani zisizomiliki chochote ndani yake."

**Arnold J. Toynbee**
Mwanahistoria wa Uingereza.



## Zama za Babaiko

"Kwa hakika sisi tunaishi katika zama za babaiko, wala hapana shaka kuwa mafanikio ya Sayansi na teknolojia zimemzidishia mwanadamu anasa na starehe lakini kwa upande mwingine haikumuongezea furaha na utulivu bali kinyume chake imemuongezea khofu, babaiko, kukata tamaa na maradhi ya nafsi yamemuondoshea maana nzuri ya maisha haya."

**Dr. Rene Dubos**
Mwanasayansi aliyepata tuzo ya Nobel




https://www.path-2-happiness.com/sw



# Haja ya dini kwa jamii mbali mbali



### Hoja yenye kuzungumza

“Kwa hakika kuna uwezekano wa kudhoofika kila kitu tunachokipenda, na kubatilisha uhuru wa matumizi ya akili, elimu, na viwanda, lakini ni muhali kufutika dini, bali itabakia kuwa ni hoja yenye kuzungumza dhidi ya ubatili wa madhehebu ya kiyakinifu (yanayotanguliza dunia na anasa zake) ambayo yanataka kumdhibiti mwanadamu katika dhiki ya uduni katika maisha ya ardhini.”

**Ernest Renan**
Mwanahistoria wa Kifaransa

Ikiwa mtu binafsi hana budi awe na dini, basi haja ya jamii mbali mbali kwenye dini ni kubwa zaidi, Dini ni ngao yenye kuikinga jamii; na hiyo ni kwa sababu maisha ya mwanadamu hayasimami isipokuwa kwa kushirikiana na watu wake katika mambo ya kheri: {…Na saidianeni katika wema na uchamngu. Wala msisaidiane katika dhambi na uadui...} [5:2],

Na ushirikiano huu hautimii ila kwa mfumo unaopangilia mahusiano yake, na kuainisha majukumu yake na kudhamini haki zao, mfumo huu hauna budi kutoka kwa yule mpole mwenye ujuzi na elimu kwa anayohitajia mwanadamu, {Asijue aliye umba, naye ndiye Mjua siri, Mwenye khabari?} [67:14]

Kila ambapo mwanadamu anapokwenda kinyume na dini, sheria yake na mfumo wake ndipo jinsi ambapo hupotea na kughibu na kudumbukia katika kiza cha shaka, upotevu, haya, taabu na mateso.

Hakuna katika ardhi yote hii nguvu ambayo ni sawa na nguvu ya dini au mtu kufuata dini katika kudhamini watu kuheshimu mfumo au utaratibu Fulani, na kadhalika kudhamini mshikamano wa jamii



**Philip Hitti**
Mwanahistoria wa Kilebanoni

### Sheria ya kweli

“Sheria ya Kiislamu haitofautishi baina ya dini na baina ya ambacho ni dunia. Sheria hiyo inaonesha mahusiano ya mwanadamu na Mwenyezi Mungu na wajibu wake kwa Mungu na kuyapanga kama inavyofanya kwa hali ya mahusiano ya mtu kwa ndugu yake mwanadamu. Na amri zote za Allah na makatazo yake –katika yanayofungamana na mambo ya dini na dunia na mengine kwenye Qur-aan na ndani yake pana ayah elfu sita au ziada ya hapo, miongoni mwa hizo ayah elfu ni kuhusu sheria.”

https://www.path-2-happiness.com/sw



na utulivu kwa mfumo wake na sababu zote za usalama na siri katika hilo ni kuwa mwanadamu anatofautiana na viumbe vingine kwa kuwa harakati zake na matendo yake ya hiari yanayotawalia uongozi wake kitu ambacho hakitokei katika usikizi wake wala uoni wake, bali ni akida ya kiimani ambayo ina adabisha roho na kutakasa kiwili wili chake na kuifanya kuwa ni mwangalizi wa siri yake kama ambavyo inakuwa ni mwangalizi wa dhahiri yake, {Na ukinyanyua sauti kwa kusema...basi hakika Yeye anajua siri na duni kuliko siri.} [20:7].

Mwanadamu huongozwa na akida iwe ni sahihi au mbovu, akida yake ikitengemaa basi mambo yake yote yatatengemaa, na ikiharibika mambo yake yote yataharibika.

Kwa ajili hiyo dini ndio ikawa dhamana bora zaidi ya kusimamisha miamala baina ya watu katika misingi ya uadilifu na usawa, na hilo likawa ni jambo ambalo halina budi katika jamii, wala hatutokuwa tumekosea tukisema kuwa dini itachukua nafasi ya moyo katika kiwiliwili cha Umma mbali mbali.

Ikiwa dini kwa ujumla inachukua nafasi hii, na leo hii mtu akiangalia ataona dini nyingine na mila mbali mbali ulimwenguni, na kila jamii yenye dini fulani hufurahishwa nayo na hukamatana nayo. Kama hali ndivyo hivyo ilivyo ni dini gani basi ambayo ndio sahihi na ambayo itamthibitishia na kumkamilishia nafsi ya mwanadamu anachotaka kukifikia?! Na ni nini vidhibiti vya dini ya haki?!



## Dini haina nafasi ya matamanio

“Tunaona katika sababu ya mapokezi ya kushangaza aliyokutana nayo Muhammad huko Madina, ni kuwa kuingia katika Uislamu kwa watu wa Madina ulianza kwa tabaka la viongozi na lengo ilikuwa ni kutibu fujo ile ambayo ilikumba jamii ya Madina na ikiteseka nayo. Sababu kubwa ni kile walichokipata ndani ya Uislamu, ambayo ni kuwepo kwa nidhamu madhubuti chini ya sheria zilizopangwa. Na matamanio ya watu kuwa chini ya utawala wa kisheria ambao umejitenga na matamanio yao.”

**Thomas Arnold**

Mustashrik (mtaalamu wa mambo ya nchi za mashariki) wa Kiingereza

## Ziko wapi akili zenu?!

“Kwa nini mna shaka ya kuwepo kwa Mungu?! Na lau si yeye basi mke wangu angenisaliti, na mtumishi wangu angeniibia.”

**Voltaire**

Mwanafalsafa wa Kifaransa



https://www.path-2-happiness.com/sw



## Vidhibiti vya dini ya haki

Mara zote kila mwenye itikadi au akida fulani ana yakini timilifu kuwa akida yake ndio itikadi iliyokuwa sahihi zaidi na ya haki kuliko itikadi nyingine, na kila mmoja anatofautiana na mwenye itikadi nyingine kwa kuthibitisha hilo; pale watu wenye itikadi za kibinadamu zilizoharibika au zilizopotea huthibitisha hilo kwa kudai kuwa wamewakuta baba zao wakifanya hivyo na ya kuwa wao huwafuata wao, Allah Ta'ala amesema, {Na kadhaalika hatukumtuma mwonyaji kwenye mji wowote ila watu wake walio deka kwa starehe walisema: Hakika sisi tuliwakuta baba zetu wanashika dini makhsusi, na sisi tunafuata nyayo zao. Akasema (Mwonyaji): Hata nikikuleteeni yenye uwongofu bora kuliko mlio wakuta nao baba zenu? Wakasema: Sisi tunayakataa tu hayo mliyo tumwa.} [43:23-24]

Na aya nyingine amesema, {Na wanapo ambiwa: Fuateni aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu; wao husema: Bali tutafuata tuliyo wakuta nayo baba zetu. Je, hata ikiwa baba zao walikuwa hawaelewi kitu, wala hawakuongoka? Na mfano wa walio kufuru ni kama mfano wa anaye mpigia kelele asiye sikia ila wito na sauti tu -- ni viziwi, mabubu, vipofu, kwa hivyo hawaelewi} [2:170-171]

Na hutoa dalili ya msimamo wao huu kwa kufuata kibubusa bila ya kutumia akili au kufikiria, au kuthibitisha kwa kutumia habari za uongo au zenye makosa, zenye kugongana ambazo hazina dalili juu ya ukweli wake, na bila ya shaka haifai kutolea hoja au dalili kwa dini hizi na mila mbali mbali.

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

Na kwa sababu haki ni moja sio nyingi, ni muhali itikadi zote hizo kuwa ni sawa, na ni muhali zote hizo kuwa sahihi katika wakati mmoja, la sivyo usawa ungekuwa unapingana, na hili halikubaliki kwa akili iliyosalimika: {…Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila ya shaka wangeli kuta ndani yake khitilafu nyingi.} [4:82].

Kama ni hivyo basi dini sahihi ni ipi? Ni vidhibiti gani ambavyo vinaweza kuhukumu kuwa moja ya itikadi hii ni ya kweli na nyingine isiyokuwa hiyo si ya kweli?!

## Vidhibiti hivi ni:-

Kwanza: Dini iwe ni kutoka kwa Mungu, yaani kutoka kwa Allah Ta'ala na hiyo iwe imekuja kupitia kwa Malaika miongoni mwa Malaika kwa Mtume ili nae afikishe kwa waja wa Allah; kwa sababu dini ya haki ni dini ya Allah aliyeumba Ulimwengu huu, na Allah Ta'ala ndiye ambaye analipa na kuwahesabu viumbe Siku ya Kiama kwa dini ambayo amewateremshia, Allah amesema: {Hakika Sisi tumekuletea wahyi wewe kama tulivyo wapelekea wahyi Nuhu na Manabii walio kuwa baada yake. Na tulimpelekea wahyi Ibrahim na Ismail na Is-haka na Yaakub na wajukuu zake, na Isa na Ayub na Yunus na Harun na Suleiman, na Daud tukampa Zaburi. Na Mitume tulio kwisha kukuhadithia kabla yake, na Mitume wengine hatukukuhadithia. Na Mwenyezi Mungu alinena na Musa kwa maneno. Mitume hao ni wabashiri na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kuletewa Mitume. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.} [4:163-165].

Na kulingana na jambo hilo ni kuwa dini yoyote ambayo mtu anajinasibisha nayo na sio



https://www.path-2-happiness.com/sw

kwa Allah ni dini batili bila ya shaka, na dini ambayo ataiendeleza mwanadamu na kuiongezea ni batili vile vile bila ya chembe ya shaka, wala mwenye kuiendeleza au kuibadilisha ni mwenye kujua yale yanayowafaa watu kuliko Allah muumba: {Asijue aliye umba, naye ndiye Mjua siri, Mwenye khabari?} [67:14]

Vinginevyo mwenye kuendeleza au kuweka sheria ni Allah Muumba mwenye kujua kinachowafaa viumbe vyake, ametakasika Allah kwa hilo: {Je, wanataka dini isiyo kuwa ya Mwenyezi Mungu, na hali kila kilichomo mbinguni na katika ardhi kimesilimu kwa kumt'ii Yeye kikipenda kisipende, na kwake Yeye watarejeshwa?} [3:83]

Na Allah akasema tena, {La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayo khitalifiana…} [4:65].

Pili: Dini hiyo iwalinganie watu kumuabudu Allah Ta'ala na kuharamisha ushirikina; hivyo basi Da'wah katika tawhidi ndio msingi wa da'wah ya Mitume yote, na ushirikina na upagani ndio ambayo inakwenda kinyume kabisa na maumbile sahihi ya mwanadamu na akili zilizoongoka, Allah Ta'ala amesema: {Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya

## Upekee wa Mungu mmoja (Tauhidi)

"Hakika ya msingi katika Uislamu ni Tauhidi kuwa Allah ni mmoja na Muhammad ni Mtume wa Allah. Ama ushirikina umewekwa pembeni. Hakuna baba wala mtoto wala mpaka kati ya ambacho ni kitukufu, na ambacho ni cha dunia, au cha Mashariki na kile cha Magharibi kuna ulimwengu mmoja tu na dini moja tu."

**Michael Hems**
Mwandishi wa Uingereza




https://www.path-2-happiness.com/sw

kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu} [21:25]

Na kila Mtume alisema maneno yafuatayo kwa watu wake: {…Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna Mungu ila Yeye. Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya Siku iliyo kuu.} [7:59],

Na kwa hilo basi dini yoyote ambayo itakiri ushirikina, au kumshirikisha Nabii au Malaika au walii au mtu au jiwe pamoja na Allah, basi dini hiyo ni batili, kwani ibada ni kwa Allah pekee hana mshirika pamoja nae, na upagani na ushirikina ni upotevu ulio dhahiri, na kila dini hata kama ikiwa kutoka kwa Allah na ikaingizwa ndani yake ushirikina basi dini hiyo vile vile ni batili, Allah Ta'ala ametupigia mfano; aliposema, {Enyi watu! Unapigwa mfano, basi usikilizeni. Hakika wale mnao waomba badala ya Mwenyezi Mungu, hawatoumba hata nzi ijapo kuwa watajumuika kwa hilo. Na nzi akiwapokonya kitu hawawezi kukipata kwake. Amedhoofika kweli huyo mwenye kutaka na mwenye kutakiwa. Hawakumuadhimisha Mwenyezi Mungu anavyo stahiki kuadhimishwa. Hakika Mwenyezi Mungu bila ya shaka ni Mwenye kushinda.} [22:73-74].






## Uumbaji wa Mwenyezi Mungu

"Kwa hakika watoto wadogo wana muelekeo uliotangulia wa kumuamini Mungu. Kwani wao huzingatia kuwa kila kilicho katika Ulimwengu huu kimeumbwa kwa sababu. Hata kama tukiwatupa watoto peke yao kisiwani na wakaishi wenyewe bila shaka watamuamini Mwenyezi Mungu."

**Justin Barret**

Mtafiti wa Chuo Kikuu cha Oxford

https://www.path-2-happiness.com/sw



**Ugonjwa wa Upotofu**

"Elimu ni dawa ya sumu ya upotofu"

**Adam Smith**
Mwanafalsafa wa Scotland

Tatu: Dini hiyo iafikiane na maumbile sahihi, Allah amesema: {Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye Dini - ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilo waumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo Dini iliyo nyooka sawa. Lakini watu wengi hawajui.} [30:30],

Na maumbile sahihi ni kila ambacho Allah amempa mwanadamu na ikawa kwake ni sehemu ya maumbile yake, kwani haiwezi kuwa dini ambayo haifai maumbile ya mwanadamu, vinginevyo basi Muumba asingekuwa na uwezo wa kuweka sheria ya dini, na jambo hii ni muhali na la kishirikina.

Nne: Dini hiyo iafikiane na akili sahihi; kwa sababu dini sahihi ni sheria ya Allah na akili sahihi ni maumbile aliyoyaumba Allah, na ni muhali sheria ya Allah na maumbile yake kugongana, Allah amesema: {Je! Hawatembei katika ardhi ili wapate kuwa na nyoyo zao za kuzingatia, au masikio ya kusikilia? Kwani hakika si macho yanayo pofuka, lakini zinazo pofuka ni nyoyo ziliomo vifuani.} [22:46]

Na Akasema, {Hakika katika mbingu na ardhi ziko Ishara kwa Waumini. Na katika umbo lenu na katika wanyama alio watawanya zimo Ishara kwa watu wenye yakini. Na kupishana usiku na mchana, na riziki anayo iteremsha Mwenyezi Mungu kutoka mbinguni, na kwayo akaifufua ardhi baada ya kufa kwake, na mabadiliko ya upepo, ni Ishara kwa watu wenye akili. Hizi Aya za Mwenyezi Mungu tunakusomea kwa haki; basi hadithi gani watakayo iamini baada ya Mwenyezi Mungu na Aya zake?} [45:3-6]

https://www.path-2-happiness.com/sw

Hivyo basi haiswihi kuwa dini ya kweli imejaa upotevu na migongano kiasi tunapata baadhi yake ni tofauti kabisa na nyingine, na huu ni mgongano wa akili sahihi, hivyo basi haiwezi kuamrisha kisha ikaja amri nyingine inayogongana nayo, wala isiharamishe jambo au kuiruhusu kwa kundi maalumu kisha kulihamisha kwa kundi jingine, au kutofautisha baina ya vyenye kufanana au kuvikusanya baina ya vyenye kugongana,

Allah Ta'ala amesema,{Hebu hawaizingatii hii Qur'ani? Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila ya shaka wangeli kuta ndani yake khitilafu nyingi.} [4:82]

Bali ni lazima iwe imejengwa kwa dalili nyingi mbali mbali zilizo wazi, Allah amesema: {…Leteni ushahidi wenu kama nyinyi ni wasema kweli.} [2:111]



### Leteni Hoja Zenu

"Mwenye busara ni Yule anayejenga Imani yake juu ya Hoja."

**David Hume**
Mwanafalsafa wa Scotland

### Mtu na tabia zake

"Mtu asiye na tabia njema ni mnyama amaeachwa huru katika ulimwengu huu."

**Albert Camus**
Mwanafalsafa wa Kifaransa





https://www.path-2-happiness.com




Tano: Dini hiyo ilingane na tabia nyema na matendo mema, Allah amesema: {Sema: Njooni nikusomeeni aliyo kuharimishieni Mola wenu Mlezi. Nayo ni kuwa, msimshirikishe Yeye na chochote. Na wazazi wenu wafanyieni wema. Wala msiwauwe watoto wenu kwa sababu ya umasikini. Sisi tunakuruzukuni nyinyi na wao. Wala msikaribie mambo machafu, yanayo onekana, na yanayo fichikana. Wala msiuwe nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameharimisha kuiuwa, ila ikiwa kwa haki. Hayo amekuusieni ili myatie akilini. Wala msiyakaribie mali ya yatima ila kwa njia ya wema kabisa, mpaka afikilie utu-uzima. Na timizeni vipimo na mizani kwa uadilifu. Sisi hatumkalifishi mtu ila kwa kadiri ya uwezo wake. Na msemapo semeni kwa uadilifu ingawa ni jamaa. Na ahadi ya Mwenyezi Mungu itekelezeni. Hayo amekuusieni ili mpate kukumbuka. Na kwa hakika hii ndiyo Njia yangu Iliyo Nyooka. Basi ifuateni, wala msifuate njia nyingine, zikakutengeni na Njia yake. Haya amekuusieni ili mpate kuchamngu.} [6:151-153]

Na Allah akasema, {Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha kufanya uadilifu, na hisani, na kuwapa jamaa; na anakataza uchafu, na uovu, na dhulma. Anakuwaidhini ili mpate kukumbuka.} [16:90]




**Kuwa Mwanahalisi**

"Mtazamo halisi katika maisha na ushauri wa kweli na kulingania kwenye hisani, huruma na mguso wa kheri wa kibinadamu, haya na mengineyo ni katika dondoo ambazo kwangu zilikuwa ni dalili kubwa za ukweli wa dini ya Uislamu."

**Jul**

Mustashrik wa Kidenimaki



**Tabia njema zinakupa raha**

"Ninachokifahamu kuwa tendo zuri ulifanyalo linalotokana na tabia njema ni lile linalokufanya baada ya hapo uhisi raha, na tabia mbaya baada ya kulifanya unapojisikia vibaya"

**Ernest Hemingway**

Mwandishi wa Kimarekani

Haisihi dini ambayo italingania uongo au mauaji au dhulma au wizi au kuhaka na kupora na kufanya uasi au mfano wa hayo.

Sita: Itengeneze mahusiano kati ya Mwanadamu na Muumba wake, na mahusiano ya viumbe kwa viumbe, Allah amesema, {Hamuabudu badala yake ila majina tu mliyo yapanga nyinyi na baba zenu. Mwenyezi Mungu hakuyateremshia hayo uthibitisho wowote. Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu tu. Yeye ameamrisha msimuabudu yeyote isipo kuwa Yeye tu. Hiyo ndiyo Dini Iliyo Nyooka. Lakini watu wengi hawajui.} [12:40]

Hivyo basi inapasa dini hiyo kutengeneza majukumu ya mwanadamu kwa Mola wake, kadhalika itengeneze mahusiano ya viumbe na watu, Allah amesema: {Muabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote. Na wafanyieni wema wazazi wawili na jamaa na mayatima na masikini na jirani wa karibu na jirani wa mbali, na rafiki wa ubavuni na mpita njia, na walio milikiwa na mikono yenu ya kulia….} [4:36].

Saba: Dini hiyo imuheshimu mwanadamu na imkirimu wala isitofautishe baina ya wafuasi wake kwa tofauti zozote zile ziwe za kijinsia, rangi au kabila; kigezo cha kufadhilishwa na ubora ni kile anachokipata mwanadamu kutoka katika kazi yake, elimu na ucha-Mungu, Allah amesema: {Na hakika tumewatukuza wanaadamu, na tumewapa vya kupanda nchi kavu na baharini…} [17:70]

https://www.path-2-happiness.com/sw

Na akasema vile vile, {Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari.} [49:13].

Nane: Dini hiyo imuelekeze mwanadamu katika njia sahihi isiyokuwa na kombo, na njia hiyo iwe ni tiba kwa mwanadamu na iwe nuru na muongozo wao, Allah amesema akielezea kuhusu majini baada ya kusikiliza kwao Qur-aan wakiambizana, {Wakasema: Enyi kaumu yetu! Sisi tumesikia Kitabu kilicho teremshwa baada ya Musa, kinacho sadikisha yaliyo kuwa kabla yake, na kinacho ongoza kwenye Haki na kwenye Njia Iliyo Nyooka.}[46: 30],

Na akasema Allah, {Na tunateremsha katika Qur'ani yaliyo ni matibabu na rehema kwa Waumini. Wala hayawazidishii madhaalimu ila khasara.} [17:82]

Nayo ni nuru na muongozo wa watu ambao unawaongoza watu kutoka kwenye dhuluma za ujinga (ujahili) na upotevu kwenda kwenye Nuru ya utiifu na furaha katika nyumba zote mbili, Allah amesema: {Enyi Watu wa Kitabu! Amekwisha kujieni Mtume wetu anaye kufichulieni mengi mliyo kuwa mkiyaficha katika Kitabu, na anaye samehe mengi. Bila shaka imekujieni kutoka kwa Mwenyezi Mungu nuru na Kitabu kinacho bainisha.} [5:15]




**Urithi bora**

"Miongoni mwa mambo muhimu ambayo Uislamu umeyarithisha Ulimwengu huu ulioendelea ni kanuni zake za dini ambazo zinaitwa Sheria. Kwa hakika sheria ya Kiislamu ni kitu cha pekee katika mlango wake, ni jumla za amri za kiungu ambazo zinaratibu maisha ya kila Muislamu katika Nyanja zote, nazo zinakusanya hukumu maalumu kuhusu ibada na mambo mengine ya kidini, kama ambayo inakusanya misingi ya kisiasa na kanuni zake mbali mbali."

**Joseph Sachacht**
Mustashrik wa Kijerumani

https://www.path-2-happiness.com/sw

Na Akasema Allah tena, {Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu. Basi anaye mkataa Shet'ani na akamuamini Mwenyezi Mungu bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti, kisicho vunjika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua. Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa walio amini. Huwatoa gizani na kuwaingiza mwangazani. Lakini walio kufuru, walinzi wao ni Mashet'ani. Huwatoa kwenye mwangaza na kuwaingiza gizani. Hao ndio watu wa Motoni, na humo watadumu.} [2:256-257].



## Hakuna Usawa

"Aina mbaya zaidi ya kukosekana usawa ni kujaribu kusawazisha kati ya vitu visivyo sawa."

**Aristotle**
Mwanafasafa wa Kigiriki



## Mtake Msaada Mwenyezi Mungu

"Pengine ingewezekana kuokoa maelfu ya wanaoadhibika kwa kupiga makelele katika hospitali za wendawazimu, lau wao wangeomba ulinzi wa Mwenyezi Mungu badala ya wao wenyewe kuingia kwenye mapigano na Nafsi zao bila ya msaada wala muokozi."

**Dale Carnegie**
Mwandishi wa Kimarekani

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

# Ni dini ipi tunayohitajia?

## Ni dini ipi ambayo tunaweza kuipitishia vigezo vya dini ya haki iliyotangulia?

Tunaweza kugawa dini mbali mbali kulingana na vyanzo vyake katika makundi mawili:

-Dini za Ardhi au za Wanadamu, sio za mbinguni wanadamu wanaziainisha na kuziendeleza wao wenyewe, sio zilizoshuka kutoka kwa Allah Ta'ala; dini hizi ni kama vile Ubudha, Uhindu, Umajusi na upagani, hizi ni dini ambao zipo mbali kabisa na dini ya kweli, dini hizi zinatokana na matamanio ya mwanadamu; {Je! Umemwona aliye fanya matamanio yake kuwa ndiye mungu wake, na Mwenyezi Mungu akamwacha apotee pamoja na kuwa ana ujuzi, na akapiga muhuri juu ya masikio yake, na moyo wake, na akambandika vitanga machoni mwake? Basi nani atamwongoa huyo baada ya Mwenyezi Mungu? Hamkumbuki?} [45:23]

Sio dini kutoka kwa Mungu, bali dini za matamanio ya watu, hivyo basi utaona kuwa dini hizi zimejaa uzushi, udajali, matabaka na migongano, Allah Ta'ala amesema, {…Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila ya shaka wangeli kuta ndani yake khitilafu nyingi.} [4:82].



### Lakini Mwenyezi Mungu ni mmoja

"Watafiti wametaabika wakiwa wanahesabu idadi ya miungu ya dini za wanadamu: Idadi ya miungu ya Wamisri wa kale ni zaidi ya miungu mia nane, na idadi ya miungu ya Kihindu ni zaidi ya miungu elfu kumi, na mfano wa ushirikina huu kwa Wagiriki na Wabudha, na mengine miongoni mwa dini za watu za ardhini."

https://www.path-2-happiness.com/sw



-Dini za Mbinguni kutoka kwa Allah, kama vile Uyahudi, Ukristo na Uislamu, na watu wenye dini hizi Muumba aliwaelekeza dini yao na kuridhia, Allah amesema, {Amekuamrisheni Dini ile ile aliyo muusia Nuhu na tuliyo kufunulia wewe, na tuliyo wausia Ibrahim na Musa na Isa, kwamba shikeni Dini wala msifarikiane kwayo. Ni magumu kwa washirikina hayo unayo waitia. Mwenyezi Mungu humteua kwake amtakaye, na humwongoa kwake aelekeaye.} [42:13]

Bila shaka dini nyingi za ardhini ni kundi kubwa la fikra mbali mbali na mkusanyiko wa wanadamu waliochagua katika yanayonasibiana na matamanio yao, lakini baada ya muda mfupi mwanadamu akagundua kuwa haifai, kwa hivyo wao wakajaribu kuziendeleza, na wao hali kadhalika kuendelea katika kupotea, sifa za dini hizi za ardhini (watu) ni hizi zifuatazo:-



**Sheria ya kweli**

"Nimefahamu na kudiriki kuwa anachohitaji mwanadamu ni sheria ya mbinguni inayoweka haki na kuondosha batili."

**Tolstow**

Mwanafasihi wa Kirusi

Ushirikina: Kila siku wanatengeneza Mungu mpya, Mungu wao anatengenezwa na mikono yao, wala hawafikiri kutokuwezekana kuwepo Mungu pamoja na Allah vinginevyo wangepigana au kugongana, Allah amesema: {Mwenyezi Mungu hana mwana yeyote, wala hanaye mungu mwengine. Inge kuwa hivyo basi kila mungu angeli chukua alivyo umba, na baadhi yao wangeli washinda wengine. Mwenyezi Mungu ameepukana na sifa wanazo msifu. Mjuzi wa siri na dhaahiri, na ametukuka juu ya hayo wanayo mshirikisha nayo.} [23:91-92]

Utabaka: Dini za ardhi zimesimama katika matabaka na kuwafanya watu kuwa watumwa; kwani watu wameweka kwa ajili yao wenyewe na sio wengine; ili wafanikiwe katika lengo lao na wawafanye wengine kuwa watumwa, Allah amesema: {Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni

https://www.path-2-happiness.com/sw



kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari.} [49:13]

Na Mwenyezi Mungu akawakataza watu kuangaliana vibaya kwa kusema, {Enyi mlio amini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao, wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao. Huenda hao wakawa bora kuliko wao} [49:11],

Hivyo basi kwa Mwenyezi Mungu hakuna fadhila au hakuna ubora wa mweupe kwa mweusi, wala kwa ukoo fulani ukilinganisha na mwingine wala kaumu fulani dhidi ya kaumu nyingine. Ama dini za ardhi (zilizoundwa na watu) zinasimama kwa misingi ya tabaka.

Kwenda kinyume na maumbile (fitra): Dini za ardhi zinakwenda kinyume na maumbile sahihi ya mwanadamu, zinasimamia katika kumbebesha mwanadamu asiyoyaweza, zipo kinyume na mazingira, na tabia ya mwanadamu, akili sahihi, kwani wafuasi wake wamekuwa mbali na njia ilionyooka na wakabadilisha, Allah amesema: {Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye Dini - ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilo waumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo Dini iliyo nyooka sawa. Lakini watu wengi hawajui.} [30:30]



## Tabaka za Kijeuri

"Mgawanyiko wa kitabaka katika dini ya Kihindu uko kama ifuatavyo: Tabaka la weupe; Hili ni tabaka la watu wa dini na wanazuoni. Tabaka la Wekundu; linakusanya maamiri na wanajeshi. Tabaka la Manjano: linakusanya wakulima na wafanya biashara. Tabaka la Weusi linahusisha mafundi mikono na viwanda. Ama tabaka la tano ambalo linafahamika kuwa ni tabaka la watu duni (Untouchable-tabaka la chini kabisa) linahusisha wenye kazi duni. Na tabaka za juu linatumikisha matabaka ya chini na matabaka ya chini yanahudumia matabaka ya juu."

https://www.path-2-happiness.com/sw

Uzushi: Ni itikati au fikra iliyosimama juu ya mawazo matupu bila ya uwepo wa sababu za kiakili, au za kimantiki au za kielimu, na dini nyingi za ardhini zina uzushi usiokuwa na dalili yoyote au hoja, wala uzushi haujengwi ila kwa uzushi wenyewe, amesema kweli Allah: {… Sema: Leteni hoja zenu kama nyinyi ni wasema kweli.} [27:64].

Migongano: Hizi ni dini ziliojaa migongano, kila kundi linasimama katika kupinga kundi jingine na huziendeleza fikra hizi pinzani, Allah amesema: {…Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila ya shaka wangeli kuta ndani yake khitilafu nyingi.} [4:82]

Ama dini za mbinguni ni neema kutoka kwa Allah ambazo Mwenyezi Mungu amewapa wanadamu ili awaongoze na kuwamulikia njia yake na kuwasimamishia hoja juu yake na kuwaepusha, upotofu, ushirikina, kwenda kinyume na maumbile (fitra) na akili kwa kuwatuma Mitume wafikishe ujumbe kutoka kwa Mola wao: {Mitume hao ni wabashiri na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kuletewa Mitume. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.} [4:165].



https://www.path-2-happiness.com/sw



## Migongano ya Kibudha

"Mabudha wanakana Mungu na wanadai (au baadhi yao) kuwa Budha ni mtoto wa Mungu, na wanapinga roho na wanaamini kuwa roho ya marehemu huingia katika mwili wa mtu mwingine."